# KUTEKELEZA USHINDI WA KRISTO DUNIANI

Sehemu ya Pili

Na Jacquelyn Fedor

Ilitafsiriwa Na David Odhiambo

Katika sehemu ya kwanza ya mfululizo huu tulijadili jinsi damu ya malaika walioanguka walioingiliana kingono na wanadamu inavyoonekana kijenetiki bado leo na athari zao zikisalia kwenye DNA yetu. Tunaweza kuona kwa nini isipokuwa kuzaliwa mara ya pili hakuna tumaini la kurudi kwenye sura ya Mungu kama katika mwanzo wetu. Hebu tuseme ukweli, mwanadamu ni aina mchanganyiko. Hatukubaki kwa jinsi yetu wenyewe. Tunaweza kufikiri kwamba malaika hawa si sehemu yetu tena, lakini sivyo.

Kulingana na Mwanzo sita, waliokuwa malaika watakatifu waliasi amri ya Mungu na kuanza kuwatamani binti wa binadamu. Kupitia kwao, tamaa ya jicho, tamaa ya mwili na kiburi cha uzima vililetwa ndani ya ubinadamu. Sifa hizi na hisia ndio kiini cha fikra za mwanadamu. Hapo awali Hawa alikuwa amechagua hekima ya Shetani badala ya hekima ya Bwana kwa hivyo mwanadamu aliweza kujihusisha na hisia hizi kwa urahisi. Malaika walivyokuwa na tamaa mbaya, mwanadamu anaendelea na tamaa hii. Kwa hivyo, damu hii huhifadhiwa kwa nguvu. Mwanadamu amejiruhusu kuvutiwa na tamaa ya jicho na tamaa ya mwili inayozaa tabia hizi tena na tena, kizazi

baada ya kizazi. Wanaume na wanawake wanatamaniana, wanaume hata wanatamani wanaume, wanawake baada ya wanawake. Wanyama wako katika hali mbaya ya kutamani!

Yote haya yalitokana na malaika na ndiyo sababu tumaini letu pekee la kuokoka ghadhabu ya Mungu mwishowe ni kuzaliwa viumbe vipya. Kwa maneno mengine, kwa maelfu ya miaka tumekuwa bila kujua tumevuka upotovu na tamaa. Tumehifadhi damu za nani?

**Waefeso 2:3** inatuambia,
3 ambao pia **sisi sote** **tulijiendesha katika tamaa ya miili yetu**, **tukatimiza matamanio** **ya mwili** na **ya akili** (Hawa alichagua ujuzi wetu), **na kwa asili Watoto wa ghadhabu**, kama vile wengine.

Shetani amebadilisha wanadamu ili kuwa mmiliki wetu. Tumekuwa tukitimiza bila kujua dhana ya Shetani ya kuwa kama Mungu kupitia ujinga wetu. Kwa kweli, kwa sababu ya uvutano wake mwovu tumejiunga katika kubadilisha uumbaji wa Mungu, kwa hiyo kuchanganya aina au spishi za karibu kila kitu kwenye sayari. Chukua wanyama kwa mfano, tunavuka farasi na punda ili kuzalisha nyumbu. Mungu hakuumba nyumbu kwa hivyo Shetani aweze kudai kiumbe kilichobadilishwa. Mimea imevukwa kwa wingi ili kuzalisha kwa wingi chakula tunachokula leo, hata maua katika bustani zetu kwa mara nyingi yamevukishwa na Shetani anadai kuwa yake pia.

Walakini, aina za zamani ni nguvu zaidi. Kadiri tunavyosonga mbali kutoka kwa uumbaji wa awali wa Mungu ndivyo magonjwa, ufisadi na uozo unavyozidi kutuathiri. Alichoumba Mungu yalikuwa kamili! Leo kila kitu kimefanywa kuhusika na kifo. Tena, hii ni sababu nyingine kwa nini nafasi pekee tuliyo nayo ni kuzaliwa mara ya pili na kuanza kutembea katika mpango wa urejesho wa Mungu ili tuweze kuweka viumbe vingine huru kutoka kwa mshiko wa adui. Shetani akiwa bwana ya ulimwengu, mwanadamu na uumbaji wote wanazidi kuwa dhaifu, wenye uwezo mdogo wa kustahimili magonjwa na maaradhi kama vile kila kitu kwenye sayari hii. Lakini kuna habari njema, Yesu alikuja kutuweka huru na haya yote! Alifanya iwe rahisi kwetu kurudishwa kwa Mungu na kurejeshwa, kufanywa upya na hatimaye hata kutokufa kwetu kurudi! Sisi kama waliorejeshwa tunaweza kuweka dunia na wote tulioumbwa kuwa watunzaji wao huru pia. Watu wa Mungu wanapoungana wanaunda mwili wa Kristo na sasa wako tayari kueneza ukweli, kuwafundisha wengine, kuharibu dhana za Shetani na kutimiza mpango wa Mungu wa ukombozi kwa viumbe.

Ili kuanza safari yetu lazima kwanza tutubu maovu ambayo sisi binafsi tulichangia kwa uovu wa wanadamu, makosa yote tuliyofanya kama sehemu ya jamii iliyobadilishwa na kumwomba Bwana atume Roho Wake mioyoni mwetu ili atuongoze kwa familia yake, Ufalme Wake, urejesho. Ni lazima tuwe tayari kujitenga na ulimwengu na watu wake, tukivunja vifungo vya nafsi na kamba za uovu ambazo hufungamana aina sawa pamoja. Hatuwezi

kuwa kama wao au kuunganishwa nao ili turudishwe na kumilikiwa na Mungu. Ikiwa tumetubu, tukamwomba Bwana mioyoni mwetu, tukatamani kupewa mwanzo mpya na kwa hiari kutengwa na ule wa kale ili kuwa kiumbe kipya sasa tuko tayari kwa kuzaliwa upya.

**Warumi 6:3-5** inaeleza kuzaliwa upya.
3 Au hamjui ya kuwa sisi sote tuliobatizwa **katika Kristo Yesu** (si vyeo,
Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, bali kubatizwa katika jina Lake, katika jina
la Yesu) **tulibatizwa katika kifo yake**? (Tunakufa kwa utu wetu wa Adamu
wa kale.)
4 Kwa hiyo tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti (si sisi
tena tulivyokuwa), ili kama vile **Kristo alivyofufuliwa kutoka kwa wafu**
**kwa utukufu wa Baba**, vivyo hivyo na **sisi tuenende** **katika upya wa**
**uzima** (kama viumbe vipya, ambavyo hatukuwekwa tena chini ya Shetani,
watu wake au ulimwengu wake).
5 Kwa maana **ikiwa tumeunganishwa pamoja katika mfano wa kifo**
**chake**, bila shaka **sisi pia** tutakuwa **katika mfano wa ufufuo wake**,

Sisi ni wapya kabisa, tayari kuanza upya, na katika nafasi ya kiroho ikiwa **1 Wakorintho 15:51-54** itaanza kutumika.
51 Tazama, ninawaambia nyinyi fumbo: Sisi sote hatutalala (au kufa), lakini
sote tutabadilishwa,
52 kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa tarumbeta ya

mwisho. Kwa maana tarumbeta italia, na wafu watafufuliwa wasiwe na uharibifu, **nasi** **tutabadilishwa**.
53 Maana sharti **huu uharibikao** **uvae kutoharibika**, nao **huu wa kufa uvae kutokufa**.
54 **Basi huu uharibikao utakapovaa kutoweza kuharibika**, na **huu wa kufa utakapovaa** **kutoweza kufa**, **ndipo** litakapotimia lile neno lililoandikwa: "**Kifo kimemezwa katika ushindi**." (Ni viumbe vipya pekee vinavyorithi ahadi hizi.)

Unaona, Shetani ana mamlaka tu juu ya waliobadilishwa. Wale waliozaliwa upya kupitia kwa Mungu ni wa familia yake tena. Kuna sheria zilizoandikwa kwenye mioyoni na akilini zao, zikiungwa mkono na enzi kuu ya Mungu, ambazo huwalinda zinapotekelezwa. Unaona kile Kristo alichotufanyia? Alilipa gharama ya uhuru wetu, ukombozi wetu kwa maisha yake mwenyewe. Tumerudishwa kwa Mungu na si tena wa jamii iliyobadilishwa ya Shetani. Yote tuliyopoteza kwa maelfu ya miaka yatarejeshwa kwetu na vilevile tunashika ushindi wa msalaba kikamilifu na kuutekeleza kwa kutumia sheria dhidi ya hali mbaya au mahitaji yetu. Kwa kuwa tumezaliwa kupitia Neno, ujuzi wa Mungu pia hutolewa tena na hekima safi na ufahamu kuhifadhiwa katika kumbukumbu zetu kwa matumizi yetu. Tukijazwa na Roho wake, kulingana na Matendo 2:38 asili yetu inaweza kurejeshwa na tabia za Mungu kupandikizwa ndani yetu kama karama, si kama tabia ya kujifunza, na Roho wa Mungu kama mshauri na mwongozo wetu.

**Matendo 2:38-39**

38 Ndipo Petro akawaambia, "**Tubuni** (tena, hili ndilo sharti la kwanza na
mwanzo wa kurejeshwa), na kila mmoja wenu abatizwe kwa **jina** la **Yesu**
**Kristo** (angalia, jina sio vyeo, mchakato wa urejesho unaendelea) kwa
**ondoleo la dhambi**, **nanyi mtapokea zawadi** ya **Roho Mtakatifu**,
39 Maana ahadi ile ni kwa ajili **yenyu** na **watoto wenyu**, **kwa wote walio**
**mbali**, kwa wote **wengi** amabo Bwana **Mungu** wetu **atawaita**."

Hii ni kwa ajili ya wokovu wa wote Shetani amewapotosha, ni kwa ajili ya kila mtu! Mwingiliano wa Roho Mtakatifu na mwanadamu ndiyo njia pekee ya kurejeshwa kabisa. Roho lazima aje juu ya mwanadamu ili kuongoza na kukomaza kiumbe kipya.

**Matendo ya Mitume 8:14-17**

14 Basi mitume waliokuwa kule Yerusalemu waliposikia ya kwamba
Samaria wamelipokea neno la Mungu, wakawatuma Petro na Yohane;
15 Walipofika waliwaombea hao waumini ili **wapokee Roho Mtakatifu**;
16 Kwa maana bado **halikuwa limwmshukia hata mmoja wao**. Walikuwa
**wamebatizwa tu** katika **jina la Bwana Yesu**.
17 Kisha **wakawekea mikono**, nao **wakampokea Roho Mtakatifu**.

Tunajuaje kama mtu amejazwa Roho? Ni ishara gani tofauti?

**Matendo 2:4** inaeleza,

4 **Wote wakajazwa Roho Mtakatifu**, wakaanza **kusema kwa lugha mbalimabali**, kama Roho alivyowajalia kutamka.

Sasa mtu wetu wa kiroho anaweza kusema na Baba tena, kwa sababu ya mwongozo wa Roho Mtakatifu na kuomba kwa njia ambayo nafsi yetu hawezi kuomba. Nafsi yetu bado yuko katika hatua za mwanzo za urejesho na angali ameathiriwa sana na mwili wetu na maarifa ya kidunia katika benki yetu ya kumbukumbu.

**I Wakorintho 14:2** inaeleza,

2 Maana **yeye anenaye kwa lugha ngeni** **hasemi** na **wanadamu** bali **husema** na **Mungu**, maana hakuna asikiaye; hata hivyo, **katika roho** hunena **mafumbo**.

**1 Wakorintho 14:1** inatuonyesha jinsi ya kufuatilia zaidi urejesho wetu.

14 **Fuatilia upendo** (unarudisha asili yetu ya kale), na kutamani **vipaji vya kiroho** (kurudisha uwezo tuliokuwa nao hapo awali), lakini hasa upate kutoa unabii (ili Mungu aweze kusema kupitia sisi ili kuwaongoza wengine).

Hebu fikiria, kupitia mwingiliano wa Roho Mtakatifu, uwezo wa Mungu, asili yake, tabia zake, tabia zake huanza kutiririka kupitia kwetu! Neno la

ujuzi, wakati huu ujuzi wa Baba, Neno la Hekima (Bibi-arusi Wake), kupambanua roho (uwezo wa kutambua kile ambacho ni cha Mungu na kile ambacho ni adui), lugha za kiroho, tafsiri za lugha za kroho na unabii (kama njia ya mawasiliano safi kati ya Mungu na mwanadamu), imani, uponyaji na miujiza (ambayo inahitajika sana kwa ajili ya kurejeshwa kwa mataifa).

**Wagalatia 5:22-23** inatuonyesha, ikiwa tutachagua Mti wa Uzima, Kristo, matunda ya maisha yetu kwa namna fulani yatakuwa kama Yake.
22 Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu,
23 upole na kiasi. Kinyume na hivyo hakuna sheria.

Tunapokuza tabia hizi kiumbe kipya kiko njiani kuwa kama Baba tena. Hapa kuna ufunguo mkubwa wa kupata ushawishi wa adui kutoka kwa maisha yetu. Shetani hana uwezo wowote kwa wale wanaoonyesha matunda haya. Yeye huwafikia waasi, waliobadilishwa. Ikiwa sisi hatuna sheria Mungu ambaye ni mwenye haki hawezi kutulinda au kuchukua upande wetu. Kutoka chini ya sheria za Mungu tumefunuliwa, uchi kiroho, na kuchuliwa kwa urahisi kwa adui.

**Waebrania 6:1-3** inatuonyesha, haya yote ni mwanzo tu wa urejesho wetu!
1 Basi, **tukiacha** kuyanena **mafundisho** ya **kwanza ya Kristo**, na tusonge **mbele kwa utimilifu**, **tusiweke msingi tena wa** **kuzitubia** kutoka **kazi**

**zisizo na uhai**, na wa kuwa na **imani kwa Mungu**,
2 wa **fundisho la ubatizo**, na **kuwekwa mikono**, na **ufufuo wa wafu**, na **hukumu ya milele**.
3 Na hili tutalifanya Mungu akitujalia.

Ikiwa tunataka kwa dhati kuona ubinadamu ukirejeshwa basi ni lazima kwa vyovyote vile twende kwenye ukamilifu kama inavyopendekezwa katika andiko hilo hapo juu. Kubaki hapa kungetuondoa katika mwili wa Kristo unaozaa mbingu mpya na dunia mpya. Tunapaswa kutaka kuwa wazee, watu wakomavu wanaoweza kutimiza sehemu yao katika kudhihirisha mpango wa Mungu wa kubadili mambo.  Kwa hivyo katika kufunga familia ya Mungu, na tuendelee kutafuta ujuzi wa Mungu wa wakati wa mwisho ili tuweze kukua hadi kufikia kimo kamili cha Kristo ili kuweka uumbaji huru, na kulazimisha ushindi, Yubile duniani.

Tembelea tovuti yetu http://www.trumpetsoftruth.com